

JINSI

YA KUHIMILI

UTANGULIZI WA JINSI YA KUHIMILI

UKOSEFU WA UHAKIKA MBELE YETU...

Tunaishi katika ulimwengu ambao haujatulia.

JINSI YA KUHIMILI

Mtazamo wa kukumbatia

Rasilimali ya kuulizia

Theolojia ya kuamini

1. **Majaribu hayana budi.** Kuwa na hali ngumu katika ulimwengu ulioanguka ni jambo la uhakika.
2. **Majaribu yaweza kututengeneza au kutubomoa.** Twaweza kuangalia upeo wa mgogoro kama tatizo lisilowezekana au nafasi kubwa.
3. **Waathiriwa wanashindwa na kusalia katika maswali ya kwa nini na kukwama katika maumivu yao.** Kamwe hawavuki hatua ya, “Mbona iwe mimi, Bwana?” na “ mbona sasa ?”

MASWALI KUTOKA KANISA LA KWANZA..

- Yesu, nifanye nini?
- Nitaikabilije hali hii na familia yangu?
- Unasemaje kuhusu tatizo langu la kiafya?
- Je, nikipoteza biashara yangu itakuwaje?
- Kuna matumaini gani ya siku za usoni?
- Niende wapi baada ya hapa?

SWALI

Ni jaribu gani huenda linakukabili sasa maishani mwako?

MTAZAMO WA KUKUMBATIA

“Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.” (Yakobo 1:2-4)

“Saburi na iwe na kazi kamilifu.” (Yakobo 1:4)

MASWALI MATATU MUHIMU YA “NINI” ...

Swali la 1: Ni nini ninachoweza kudhibiti ulimwengu wangu ukiporomoka?

Jibu: Mtazamo

Swali la 2: Lazima nifanye nini ili niweze kufaulu siku ya leo?

Jibu: Vumilia

Swali la 3: Nina tumaini nini kuhusu kesho?

Jibu: Amini kuwa Mungu atachukua yale mabaya ya kuzidi tunayopitia leo na ayatumie kwa wema.

Yakobo anatuelekeza kuwa tuiache saburi ikamilishe kazi yake ili tukomae na kukamilika (neno la Kiyunani telios), “bila kupungukiwa na kitu chochote.” (Yakobo 1:4)

“Wale Mungu aliowajua tangu mwanzo, pia aliwachagua tangu mwanzo, wapate kufanana na mfano wa Mwanawe.” (Warumi 8:29)

Kitabu cha Waebrania kinatusimulia kuhusu mashujaa wengi wa Imani ambao hawakuwahi kuona utimilifu wa ahadi kuu za Mungu. Iliwabidi waamini tu. Na kwasababu walifanya hivyo—kwa sababu walitazama kwa matumaini yaliyopita hali zao za wakati ule—“ulimwengu haukustahili kuwa nao.”
(Waebrania 11:38)

Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia wampendao
(Yakobo 1:12)

MTAZAMO KUHUSU MAUMIVU

1. Mungu anatumia hali ngumu za maisha kutufanya tukomae kwa sababu tunalazimishwa kumtegemea Yeye katika kiwango kipa.
2. Tumeachishwa kutoka kwa mambo yanayoendelea maishani na kulazimishwa sasa na kuchunguza upya yale tunayothamini, yale tuyapayo kipaumbele, kujitoa na wakati ujao.
3. Majaribu yanaturuhusu tushuhudie moja kwa moja uhalisia na uwezo wa Mungu.
4. Majaribu yanatumika kama ushuhuda wa ajabu kwa ulimwengu usioamini.
5. Tunakuwa wasiogusika, wanaojali, wenye huruma, watu waliofanana na Kristo.

SWALI

Ni mtazamo gani katika maisha yangu unahitaji mabadiliko ili niweze kukua wakati ninapitia majaribu?

RASILIMALI YA KUULIZIA

WATU AINA MBILI...

1. Watu wanaoendelea kuuliza mbona. Wanatazama ndani na kuzama katika kujisikitikia.
2. Watu wanaolenga swala la nini wanahitaji kufanya ili kuwa bora. Hao ndio wanaofaulu.

MASWALI MATATU YA “NINI” ...

1. Ni nini ninachoweza kudhibiti? mtazamo wangu.
2. Lazima nifanye nini ili niweze kufaulu siku ya leo?
vumilia.
3. Nina tumaini nini kuhusu kesho?
Mungu mwenye nguvu zote, Mungu ajuaye yote ameahidi kuchukua hali ngumu zaidi ninayopitia katika maisha haya aigeuze kuwa wema kwangu, katika maisha haya au mbinguni.

NINI CHA KUFANYA WAKATI UMEKWAMA

“Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa. Ila na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Mtu wa nia mbili husita-sita katika njia zake zote.” (Yakobo 1:5-8)

Ofa ya Mungu: Hekima isiyo ya ulimwengu

Jukumu letu: Lazima tuiombe Hiyo

Mtazamo wa Mungu: Kuwa wazi na mkarimu

SHARTI LILE MOJA

“Lazima uamini wala usiwe na shaka...” (Yakobo 1:6)

Mtu anayeomba ili ajue mapenzi ya Mungu kama habari tu, jambo la kuwazia, pasikuwa na kujitolea kokote kwa kufuata hupata jibu linaloweza kubashirika.

“Mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana.”
(Yakobo 1:7)

KATIKA WAKATI WAKO WA UHITAJI

1. Kiri kuwa umekwama.
2. Tambua kuwa huwezi kufanya chochote kwa nguvu zako..
3. Omba akupatie hekima isiyo ya ulimwengu.
4. Kuwa na moyo wa kufanya chochote hekima Yake itakutaka ufanye.

DHAMIRA INAYOPATIKANA MARA KWA MARA KATIKA MAANDIKO NI...

“BWANA yu karibu nao waliovunjika moyo, Na waliopondeka roho huwaokoa.” (Zaburi 34:18)

Anatualika tukikaribie kiti chake cha neema kwa ujasiri, -“ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji” (Waebrania 4:16)

Mungu anakupatia rasilimali ya thamani kuu zaidi ulimwenguni:

Hekima

Yake

Anakuongoza katika hali zako unazopitia kwa neema ya kutosha kuweza kushughulikia kila siku na ahadi ya kufanya kila kitu kiwe kwa wema wako.

MASWALI

1. Ni wapi unahitaji hekima ya Mungu isiyo ya kawaida?
2. Je kuna mahali popote huenda unaweza kataa msaada wa Mungu kwa kukataa kufanya kile Yeye anakutaka ufanye?

THEOLOJIA YA KUAMINI

Shetani hutumia “ **uvunjikaji wa moyo** ” kama kifaa chake chenye nguvu zaidi

KUUA JOKA LA UVUNJIKAJI WA MOYO

Kuvunjika moyo husababisha tumaini limomonyoke na kutufanya tukate tamaa. Kidogo kidogo, hutushawishi kuwa hatuna nguvu, kuwa hakuna kitakachobadilika, kuwa haina maana yoyote kujaribu. Ni ile hisia inayolegeza msimamo na kuingiliana, ichukuayo njia za mkato, na kufanya kuacha kuonekane ndilo chaguo letu sahihi.

KUPITIA UPYA

Mpango wa Mungu unaanza na **mtazamo** : **Kuvumilia kwa Furaha**

Mtazamo huo huleta **matokeo** : **kuwa tutakuwa wakomavu, watimilifu, bila kupungukiwa na chochote.**

Mungu pia hutupa **rasilimali** ya thamani ya juu zaidi: **Hekima isiyo ya kawaida**

MUNGU ANATUPATIA THEOLOJIA— MTAZAMO WA KIUNGU, PICHA KUBWA YA UKWELI KUHUSU MAISHA, HALI NA SIKU ZETU ZA USONI.

“Lakini ndugu asiye na cheo na afurahi kwa kuwa ametukuzwa; bali tajiri kwa kuwa ameshushwa— kwa maana kama ua la majani atatoweka. Maana jua huchomoza kwa hari, huyakausha majani; ua lake huanguka, uzuri wa umbo lake hupotea; vivyo hivyo naye tajiri atanyauka katika njia zake.” (Yakobo 1:9-11)

“Heri mtu anayevumilia wakati wa majaribu, kwa sababu akiisha kushinda hilo jaribio atapewa taji ya uzima Mungu aliyowaahidia wale wampendao.” (Yakobo 1:12)

MAISHA YANAPITA

“Jua huchomoza kwa hari, huyakausha majani; ua lake huanguka, uzuri wa umbo lake hupotea.” (Yakobo 1:11)

USIKATE TAMAA!

Kwa mtu yule atakayeshinda hilo jaribio, “mtu huyo atapewa taji ya uzima.” (Yakobo 1:12)

“Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.” (2 Wakorintho 4:16-19)

KUVUMILIA NYAKATI ZA TABU

1. Pata mtazamo wa Mungu kwa hali zako
2. Pata mtazamo wa Mungu kwa siku zako za usoni.
3. Pata mtazamo wa Mungu kwa msukumo wako au motisha yako.

WEWE SI MUATHIRIWA

1. Je, imani yangu ipo katika vitu viharibikavyo au iko katika vitu ambavyo ni vya kudumu?
2. Je, tumaini langu laamuliwa na ukubwa wa shida zangu au na uhakika wa ahadi za Mungu?
3. Je, msingi wa motisha yangu ni kumpenda Kristo au ni kupata afueni tu?

Kuna JINSI ya kuhimili, na Mungu anataka ujifunze jinsi hiyo.

PUNDE UNAPOANZA TU KUVUNJIKA MOYO, KUMBUKA IMANI, TUMAINI NA UPENDO.

1. Imani hukita moyo wako katika ukweli halisi kuwa Mungu anadhibiti hali.
2. Tumaini hukukumbusha kuwa wewe ni mwanawe na kuwa ana mahali, mpango na ahadi kwa ajili yako.
3. Upendo huondoa umakinifu wako kwenye kuangalia tabu na kuuelekeza kwenye tunu ya kuteseka kwa ajili ya Mungu kama namna ya kuonyesha kujitolea kwako.

HATUA ZINAZOFUATIA

[illegible]

Pitisha kadi yako yenye
nambari ya siri, kwenye mwale
wa elektroniki ili kupata
rasilimali zaidi

